AckySHINE.com

# Je, mvulana anaweza akafikia mshindo kwa njia ya kusugua uume na vidole na kuna madhara gani ukisugua uume na vidole?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, mvulana anaweza akafikia mshindo kwa njia ya kusugua uume na vidole. Anaposuguliwa uume na vidole, msisimko wa mwili unaongezeka na damu zinaingia kwenye mishipa ya damu katika uume.

Basi, uume unasimama na mara nyingi ukiendelea kusuguliwa mvulana anamwaga mbegu zake. Kusugua uume ni njia salama ya kumaliza ashiki ya kutaka kujamii ana. Hakuna madhara yoyote ya kiafya wala kiakili kama uume unasuguliwa. Watu wengine wanasema kwamba kupiga punyeto inasababisha shida ya kisaikolojia kutokea na nguvu ya kiume kupungua. Wengine wanasema kwamba mtu anayepiga punyeto atashindwa kujamii ana na mwanamke. Lakini si kweli, ni uvumi potofu tu.